Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

25/= Ksh

# Al-Hudaa [Uongofu]

# الهدى

Volume 4, Issue 2

6th Dhul-Hijjah 1431

12th November, 2010

## Hukmu Zenye Kuhusiana Na ‘Idd

Mtayarishi: Sheikh Muhammad al-Jibaaly

Yaliyomo

Hukmu Zenye Kuhusiana Na ‘Idd 1– 3

Ibada Ya Kuchinja 3 – 4

### SHEREHE ZA ‘IDD

*Al-’Idd* ni siku yoyote ya mkusanyiko. Ni neno lililotokana na *‘aada* (maana yake imerudi), kwa sababu watu huwa na tabia ya kurudi kwenye hiyo siku. Baadhi yao wamesemwa yakuwa imetokana na *’aadah* (mazoea au mila) kwa sababu watu wameizoea. Wingi wake ni *‘ayaad*. Amesema Ibn ul-Arabi: “Imeitwa *‘Idd* kwa sababu inarudi kila mwaka na furaha mpya.”

Ibn al-’Aabideen amesema: “Masiku ya ‘Idd yameitwa hivyo kwa sababu Allaah (سبحانه وتعالى) huwaletea upya fadhla Zake. Huzigawanya Baraka zake hizi kwa waja wake. ‘Idd ul-Fitr humaliza kujizuiya na chakula, na huingiza malipo ya Swadaqaat ul-Fitr. Na ‘Idd ul-Adh-ha ni alama ya ukamilishaji wa Hajj na Uchinjaji. Vilevile furaha nyingi na kurudi tena kwenye uchangamfu katika masiku hayo.”

### ‘IDD MBILI NI REHMA ZA ALLAAH

Anas (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwakuta watu wa Madeenah wakisherehekea siku mbili ambazo ubora wake wameuendeleza kutoka kwenye zama za Jaahiliyyah. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawaambia: *“Kwa hakika Allaah amewabadilishia na siku zilizo bora; ‘Idd ul Adh-ha na ‘Idd ul Fitr.”*

Hizi ndizo siku Kuu za wafuasi wa Mtume wa Allaah (صلى الله عليه وسلم) ambae aliyebarikiwa na Allaah na yaliyo “bora”. Ni jambo la kusikitisha kuona yakwamba Waislamu wengi wanaodai kufuata Sunnah na huku wanapinga kuhusu “ubora” wa siku hizi kwa kujihusisha na sherehe za ki-desturi za kimila mbali na zile ambazo Mola wetu (عز وجلّ) alizotubariki nazo.

### KUPIGA MATWARI

‘Aaisha (رضي الله عنها) amesema: “Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliingia (nyumbani kwangu) na palikuwa na wasichana wawili wakiimba wimbo wa *Bu’aath* (mashairi ya zama za Jaahiliyyah) [na huku wakipiga matwari], kwahiyo akajibwaga kitandani na akageuza uso wake kando. Kisha Abu Bakr nae akaja ndani na akanikaripia kwa kusema, “Zumari ya Shaytaan mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)?!” Mara Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamkabili na akamwambia, *“Wachana nao. [Kila watu wana ‘Idd zao, na hii ni ‘Idd yetu.”*

Kuimba pamoja na kupiga *duff* (matwari) ni sampuli ya lahw (upuuzi)ulioruhusiwa kwa wanawake. Ruhusa hii haikupewa wanaume. Vilevile, hicho walichoruhusiwa wanawake kutumia kikomo chake ni hilo *duff*, na makisio yoyote ya kwenye vyombo vyengine vya miziki ni batili. Kuna matukio aina tatu ambayo *Sharee’ah* imewaruhusu wanawake kutumia *duff*;

1. Katika siku za ‘Idd.
2. Katika siku za Harusi

3.Kusherehekea kuwasili kwa mtu Muheshimiwa.

Kwenye matukio kama haya, kuwasikiya wanawake wakipiga *duff*, na nyimbo wanazoimba pamoja nayo ni mambo waliyoruhusiwa kwa wanaume, kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwahi kufanya hivyo na akaliruhusu jambo hilo kama tuonavyo kwenye Hadeeth ya hapo juu. Hakukuwahi kuwa na riwaya baada ya hapo kuonyesha yakwamba Maswahaba walikhalifiana juu ya kuruhusiwa huku (Hii haimaanishi yakwamba wanaume na wachanganyike pamoja na wanawake wasiohusiana!) pia hakuna riwaya kuonyesha yakwamba maswahaba wanaume wenyewe walipiga *duff*. Hii ndiyo sababu tukasema yakwamba kupiga matwari kunaruhusiwa kwa wanawake kwa sababu huwo ni katika mtindo wao na Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaruhusu kufanya hivyo, lakini Allaah (سبحانه وتعالى) aliharamisha wanaume kuwaiga wanawake na wanawake kuwaiga wanaume. Rai hii ndiyo waliyo nayo jamuhuri ya wanavyuoni, sampuli zake ni kama zifuatazo.

### 1. SHEIKH UL ISLAAM IBN-TAYMIYYAH:

Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliruhusu baadhi ya sampuli za *lawh* kwenye matukio ya harusi na mfano wake, kama kuruhusiwa mwanamke kupiga duff katika wakati wa harusi na sherehe zake. Amma kwa upande wa wanaume, katika wakati huo, hakuna yoyote miongoni mwao anayeruhusiwa kupiga duff wala hata kupiga makofi. Bali, imethubutu kwenye swaheeh mbili yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: *“Kupiga makofi ni kwa wanawake, na tasbeeh ni kwa wanaume.”* na *“Mwanamume mwenye kujishabihisha na wanawake amelaaniwa, na mwanamke mwenye*

*(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)*

# Hukmu Zenye Kuhusiana Na ‘Idd

*(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)*

*kujishabihisha na mwanamume amelaaniwa*.” Na kuimba kukiandamana na kupiga *duff* ni miongoni mwa desturi za wanawake, na watu wema waliotutangulia wamempachika mtu mwenye kufanya hivyo na jina la *khanithi*.”

### 2. IBN QUDAAMAH:

Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaruhusu wanawake kupiga *duff* kwenye harusi na akawaruhusu mahali pengine, kwahivyo uharamu wake haukubainishwa isipokuwa atakaelipiga (hilo *duff*) ni mwanamume , ambapo katika hali hiyo, atakuwa amejifananisha na wanawake ...”

### 3. IBN HAJAR AL-HAYTHAMEE:

Katika kuyasherehesha maneno ya Ibn Qudaamah yaliyotangulia, alisema, “Ni wazi yakwamba maneno yake yalikusudia uharamu wake (kwa wanaume).”

### 4. IBN HAJAR AL-ASQALAANI:

Katika kusherehesha Hadeeth (ambayo anayodai kuwa ni *dha’eef*): “*Tangazeni (amri kwa wengi) nikaah na Mupige (amri kwa wengi) duff*.” Ambayo hutumiwa na baadhi ya watu kuthibitisha hayo, kwani kupiga duff kumetajwa kwa ujumla, kwahivyo wanaume pia wanaweza kufanya hivyo kama wanawake, (ingawaje mpokezi wake ni mwanamke) akasema: “Katika kutafuta kuyathibitisha kwamba ’ ...na mupige duff, halikuwa ni makhsusi kwa wanawake ni hoja yenye udhaifu sana, na ahaadeeth zinathibitisha kwa nguvu yakwamba ruhusa ilikuwa ni kwa wanawake. Jambo hilo haliwaepushi wanaume kutokana na makatazo hayo ya kujifananisha nao (wanawake).”

### 5. AL-MUBAARAKPURI:

Katika kuisherehesha hadeeth hiyo hiyo, alisema: “Ma-fuqahaa (wanavyuoni) wamesema: ‘*Duff* lililokusudiwa hapa ni lile lisilokuwa na kengele (vibamba), kama alivyotaja Ibn Hammaam.” kisha akasema, “Vilevile, kuimba kunaruhusiwa katika wakati wa harusi kwa wanawake, lakini hakuruhusiwi kwa wanaume.”

Mambo ya kawaida katika zama zetu ni mandhari mbaya iliyotabiriwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) ambapo wake kwa waume hukusanyika pamoja kujipumbaza nafsi zao kwa ala za miziki na vitendo vyengine vya haramu.”

Si kuleta tabia hii mbaya ya upotofu kwenye sherehe za Siku Kuu za Waislamu tu, bali wao hujaribu kwa vicheko kuyahalalisha kwa madai yakwamba hadeeth hiyo iliyotangulia inawaruhusu kushiriki. Imedhihiri wazi kutokana na tuliyosema yakwamba mwanamume mwenye kupiga duff amejifanya mke. Sasa mwanamume mwenye kupiga congo kwenye Musalla na huku akiyumba akiwa chakari kwa sauti yake, kwa hakika ni muovu zaidi.

## SUNAN ZA ’IDD MBILI

**GHUSL:** Riwaya kumuhusu Mtume (صلى الله عليه وسلم) akitekeleza Ghusl kwa swala za ’Idd ni dha’eef. Hatahivyo, imepokewa yakwamba Waislamu wa awali walifanya hayo; kwa mfano:

**A.Ibn ’Umar (رضي الله عنه):**

Alikuwa akitekeleza ghusl siku ya Fitr kabla hajenda katika musalla.

**B. ‘Ali (رضي الله عنه):**

Mtu mmoja alimuuliza kuhusu ghusl, akamwambia, “Waweza kutekeleza ghusl kila siku ukitaka.” Akasema, “Si hivyo, lakini (siku ambazo mtu atahitajika) kutekeleza ghusl.” Akasema (رضي الله عنه), “Siku ya ljumaa, siku ya ’Arafah, siku ya Nahr, na siku ya Fitr.”

**C. Sa’eed Bin al-Musayyib (رضي الله عنه): amesema:**

“Kuna Sunnah tatu za Fitr: Kutembea kuelekea kwenye musalla, kula kabla hujenda, na kutekeleza ghusl.

## KUJIKWATUA KWA AJILI YA ‘IDD

Amepokea Ibn ‘Umar (رضي الله عنهما): “Umar alileta kilemba cha hariri kutoka sokoni, akampelekea Mjumbe wa Allaah, na akamwambia, ‘Ewe Mjumbe wa Allaah, chukuwa hiki na ujipambe nafsi yako katika siku ya ‘Idd na siku utakapofanyiwa ziyara na wajumbe tafauti.’ Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: “*Nguo hii ni ya wale wasiokuwa na fungu (katika siku ya Qiyaamah)*.” Kisha baada ya muda mrefu kupita, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akampelekea ‘Umar kilemba cha hariri. ‘Umar akaja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kilemba akamwambia, “Ewe Mjumbe wa Allaah! Wewe ulisema yakwamba nguo hii ni ya wale wasiokuwa na fungu (katika siku ya Qiyaamah), na kisha ukaniletea mimi!” Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: “*Kiuze na utekeleze mahitaji yako kwa hicho*.”

Hadeeth hii ni dalili yakwamba Maswahaba walikuwa wakivalia vizuri katika Siku Kuu zao, na Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwakataza kufanya hivyo. Kwa hakika Ibn Hajar amesema: “Ibn Abu ad-Dun’yaa na al-Baihaqee wamepokea, kwa isnadi iliyo swaheeh ya wapokezi kutoka kwa Ibn ’Umar, yakwamba alikuwa akivaa nguo zake nzuri katika siku za ’Idd mbili ...” Akanukuu Ibn Qudaamah, “Na hili lathibitisha yakwamba walikuwa wakiruhusiwa kujikwatua kwenye masiku haya. Amesema Maalik, ’Niliwasikiya wanavyuoni wakieleza kuhusu kupenda kujipaka manukato na kujipamba katika kila ’Idd.’”

Ibn al-Qayyim nae akasema: “ Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akuvalia nguo zake nzuri akenda kuswali. Alikuwa na nguo makhsusi akizivaa kwa ’Idd mbili na siku ya ljumaa. Siku moja alivaa kilemba cha rangi ya kijani na mara nyengine akavaa cha rangi ya nyekundu—lakini si cha rangi nyekundu mbichi kama watakavyodhani watu wengine, lakini kilikuwa na maridadi za rangi nyekundu kama kilemba cha ki-Yemen.”

Al-Maqtari akanukuu: “Miongoni mwa mapambo ni kujitia wanja, mafuta mazuri na kuvaa *’amaamah* au kuvaa kofia. Na Waislamu wanaume

*(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)*

# Hukmu Zenye Kuhusiana Na 'Idd

*(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)*

wasiwache vichwa vyao wazi, kwa vile kuwa hivyo ni katika mila za Wazungu wa Ulaya kama ilivyotajwa na Sheikh al-Albaani katika *Tamaam al-Minnah*."

## KULA AU KABLA YA KUONDOKA

Kutoka kwa Anas Bin Maalik (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa hatoki kwenye siku ya Fitr mpaka kwanza ale tende."

Kutoka kwa Buraydah Bin al-Haseeb (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa hatoki kwenye siku ya Fitr mpaka kwanza ale. Katika siku ya Nahr (siku ya kuchinja) alikuwa haanzi kula mpaka akirudi ndipo anapokula mnyama aliyechinjwa."

## KWENDA KATIKA MUSALLA

Sunnah ni kuswali swala za 'Idd nje kwenye kiwanja. Hapa nje pa mkusanyiko kwenye kiwanja panaitwa musalla.

Amesema Abu Sa'eed al-Khudhree amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitoka siku ya Fitr na siku ya Adh-ha kuelekea kwenye musalla na jambo la kwanza alilofanya alipofika hapo lilikuwa ni kuswali."

Ibn al-Hajj al-Maalik amesema: "Sunnah imethibitisha Swalaat ul-'Eidayn kwenye musalla, kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema, *'Swala moja katika msikiti wangu ni bora kuliko swala elfu moja katika msikiti mwengine isipokuwa katika msikiti wa Masjid ul-Haraam."* Kisha baada ya kuitambua fadhla hii tukufu, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikwenda kuswali nje (kwenye musalla) akajiepusha kuswali (ndani ya msikiti).

## KURUDI KUTOKA KATIKA MUSALLA KWA NJIA TAFAUTI

Kutoka kwa Jaabir Bin 'Abdillaah(رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akichukuwa njian tafauti katika siku za 'Idd."

Ibn al-Qayyim amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akichukuwa njia tafauti katika siku za 'Idd. Alikwenda kwa njia moja na kurudi kwa njia nyengine. Wamesema yakwamba sababu ya hii ni kuwaamkuwa watu kwenye njia zote hizo mbili. Wengine wamesema yakwamba ni kupata baraka zilizopo za njia zote mbili. Baadhi nyengine wamesema ni kwa kuubainisha (kwa takbeer n.k) Uislamu, na wengine wamesema - na msemo huu wao ndio bora zaidi - ni kwa sababu zote hizi zilizotajwa na nyengine ambazo yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) azijuazo."

## MWENDO WA KUTEMBEA

'Ali (رضي الله عنه) amepokewa kuwa amesema: "Miongoni mwa Sunnah ni kwenda kwenye 'Idd kwa kutembea."

## KULETA TAKBEER KATIKA 'IDD MBILI

Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Na (anakutakieni) kumtukuza Allaah kwa kuwa amekuongozeni, ili mpate kushukuru."** [al-Baqarah 2:185]

Imethubutu yakwamba pindi Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Alipokuwa akenda katika siku ya Fitr, alikuwa akileta Takbeer mpaka afike kwenye musalla, na mapaka amalize kuswali. Amalizapo kuswali, hunyamaza kuleta takbeer."

Mwanachuoni wa Hadeeth, Sheikh al-Albaani amesema: "Katika hadeeth hii ni dalili ya kuruhusiwa kwa yaliyo kawaida miongoni mwa Waislamu wengi ya kuleta takbeer kwa sauti wanapoelekea kwenye musalla ... Kulingana na sisi, kuleta takbeer kwa pamoja (sauti moja) kama wanavyofanya watu wengi ni jambo ambalo halikuamrishwa. Kila sampuli ya Dhikr imeamrishwa iwapo itamkwe kwa sauti au kuletwa kimya, lakini hakuna ruhusa ya kuleta Dhikr kwa sauti moja. Kwahivyo, hili ni **ONYO** kali dhidi ya kitendo hicho..."

Ama kuhusu wakati maalum ambao takbeer huanzishwa, ni wakati wote bila ya kuwa makhsusi. Maadamu hilo ndilo lililosemwa na Imaam al-Bukhaari katika *Kitaab ul -'Eidayn* cha Swaheeh yake:

**ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO**

# IBADA YA KUCHINJA

*(Endelea Kutoka Vol. 4, Issue 1)*

Hadithi hizi pamoja na nyengine zilo sahih zaonyesha mambo yafuatayo kuhusu umri unaoruhusiwa wa wanyama (vichinjo).

a) Ngamia, Ng'ombe na Mbuzi wanaohitajika kutimia **Thaniyy** ama zaidi.

b) Kondoo awe ametimia **Jatha'** au zaidi.

### Rangi Ya Kichinjo (Wanyama)

Wanyama weupe (weupe wa kuiva) wanapendekezwa zaidi kuliko weusi kwa kuchinja. Abu Huraira (r.a.a.) akapokea hadithi kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alosema: **"Damu ya mbuzi mweupe inapendwa zaidi na Allaah kuliko ile ya mbuzi weusi wawili."**

### Nidhamu Za Kuchinja

#### Huruma Kwa Wanyama

Kabla ya kumkurubia mnyama alokusudiwa kuchinjwa, inampasa mtu kukinoa kisu chake. Kisha amchinje kwa haraka bila ya kumcheleweshea maumivu. Shaddaad Bin Aws (r.a.a.) akatuhadithia yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): **"Allaah (s.w.t.) ametuamrisha kufanya wema katika mambo yote. Kwahivyo hata unapouwa, tekeleza hivyo kwa njia nzuri. Na unapochinja, tekeleza kwa uzuri. Inampasa mmoja wenu kunoa kisu chake na amtulize kichinjo chake (kuharakisha Uchinjaji)."**

### Jinsi Ya Kumchinja Mnyama

Swahaba Anas Bin Malik (r.a.a.) akatuhadithia yakwamba Mtume صلى الله (عليه وسلم) alichinja kondoo wawili madume wenye rangi nyeupe na pembe kubwa. Aliwachinja yeye mwenyewe binafsi. Anapomchinja, humlaza chini kisha akamkanyaga shingo upande wake na akasema: **"Bismillaah, Wallahu Akbar (kwa jina la Allaah, Allaah ni Mkubwa)."** Na 'Aaisha (r.a.a.) akahadithia yakwamba: "Mtume wa Allaah صلى الله (عليه وسلم) aliagiza aletewe kondoo

*(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)*

mwenye pembe akiwa na rangi nyeusi miguuni na machoni. Alipoletewa akaniambia, *"Ewe 'Aaisha nipatie kisu."* Kisha akasema, *"Nenda kakitie makali (kakinoe)."* Nami nikafanya hivyo kisha nikampa. Akamlaza chini yule kondoo na akamchinja akisema: *"Bismillaah, Ewe Allaah, takabali kutoka kwa Muhammad, Ahli ya Muhammad na Umma wa Muhammad."* Na hapo tena akamchinja."

Vile vile hadithi hizi zinatuonyesha yakuwa kondoo hachinjwi hali ya kuwa ameketi au amesimama bali huchinjwa hali yakuwa amelazwa. Ama kuhusu Ngamia, ikapokewa kutoka kwa Ibn 'Umar (r.a.a.) kuwa sunnah ya Mtume صلى (الله عليه وسلم) ni kumchinja Ngamia hali ya yakuwa amesimama kwa miguu mitatu na mguu mmoja wa mbele wa kushoto umekunjwa na kufungwa.

Pia, ushahidi zaidi unaonyesha kuwa mchinjaji atamke tasmiyah (kusema: Bismillaah) na takbir na amkanyage upande mmoja wa shingo ili kurahisisha uchinjaji. Katika tukio hilo (la uchinjaji) Mtume (صلى الله عليه وسلم) alichinja sadaqa yake yeye mwenyewe. Ni bora mtu kuitekeleza sadaqa yake kwa mikono yake mwenyewe. Lakini, yaruhusiwa mtu kumuakilisha mwenziwe kwenye kuchinja kama ilivyotajwa kwenye hadithi ifuatayo ya Ali (r.a.a.) hapo chini.

## Kugawanywa Kwa Nyama

**Ni Vipi Kugawanya Nyama**

Hapo awali, Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwakataza watu kuiweka nyama au kuila kwa zaidi ya siku tatu. Kisha baadae akawaruhusu: 'Aaisha (r.a.a.) akapokea hadithi kutoka kwa Mtume صلى (الله عليه وسلم) kuwa amesema: **"Hapo awali niliwakataza kuiweka nyama muliochinja zaidi ya siku tatu kwa sababu ya mabedui masikini waliokuwa wakija Madina. Lakini sasa nawaambia: Kuleni, wekeni na toeni kama sadaqa."**

Hii yaonyesha yakwamba mtu anaweza kula baadhi ya sadaqa yake, atoe baadhi kama sadaqa au tunu na pia aeke sehemu. Hapana kiwango maalumu kuhusu vigawanyo. Aya zifuatazo zinaonyesha wale wanaostahiki kugawiwa bila ya kushurutisha vipimo: **"Na kuleni katika wanyama hao na mlisheni mwenye shida alie fakiri..."** **"Kuleni katika hao na mulishe mafakiri wanao omba na wanaorondearonde bila ya kuomba..."**

Kwahivyo ni bora mtu angalau aonje sehemu ya sadaqa yake, na awape masikini kiasi alichokieka. Hivyo ndivyo alivyofanya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama ilivyo kwenye hadithi iliyopokewa na 'Ali (r.a.a.) hapo chini.

**Kuuza Sehemu Ya Sadaqa?**

Hairuhusiwi kuuza sehemu yoyote ya mnyama aliechinjwa kwa sadaqa. Abu Huraira (r.a.a.) akatuhadithia ya kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: **"Yeyote anaeuza ngozi ya kichinjo chake basi (sadaqa yake) haikubaliwi."**

Hata mchinjaji mnyama (anaesafisha na kukata) asichukue nyama hiyo kama malipo yake. Ali Bin Abu Taalib (r.a.a.) akasema: **"Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameniamrisha mimi nimchinjie Ngamia wake, na nitoe nyama, ngozi na matumbo kama sadaqa, na mchinjaji asichukue chochote na akasema, 'Tutamlipa sisi wenyewe (kando)'."**